# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

Simu. 03-3425-4531 FAX. 03-3425-7844
Barua pepe: tzrepjp@tanzaniaembassy.or.jp
tokyo@nje.go.tz

UBALOZI WA JAMHURI YA
MUUNGANO WA TANZANIA
21-9, KAMIYOGA 4-CHOME.
SETAGAYA-KU, TOKYO 158-0098

## FURSA YA MAFUNZO YA SAYANSI YA DATA NA AKILI MNEMBA (AI)

Ubalozi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nchini Japan unapenda kutoa taarifa kuhusu fursa ya mafunzo kwa njia ya mtandao kwa wanafunzi kuanzia ngazi ya sekondari hadi shahada ya uzamivu, yanayotolewa na Chuo Kikuu cha Tokyo kupitia Maabara yake ya Matsuo-Iwasawa. Mafunzo hayo yanahusu Sayansi ya Data na Akili Mnemba (AI), ikiwemo Python na Ujifunzaji wa Mashine (Machine Learning), pamoja na matumizi ya data katika biashara. Mafunzo haya yanatolewa bila malipo kwa washiriki wenye sifa.

Muda wa Mafunzo: 17 Septemba – 17 Desemba 2026 (takribani miezi mitatu).

Mada zitakazofundishwa ni pamoja na Sayansi ya Data, Python, Ujifunzaji wa Mashine, uchakataji na uwasilishaji wa data, SQL na matumizi ya Sayansi ya Data katika biashara. Washiriki watakaokamilisha masharti ya programu watatunukiwa cheti.

Sifa za Waombaji: Wanafunzi kuanzia ngazi ya sekondari hadi shahada ya uzamivu, wanaosoma katika taasisi ya elimu inayotambuliwa. Mwombaji anatakiwa kuwa mwanafunzi wakati wa kuanza kwa programu, kuwa na uwezo wa kujifunza kwa kujitegemea na kuwa tayari kushiriki na kukamilisha mahitaji ya mafunzo.

**Utaratibu wa Kuomba:**

(i) Sajili barua pepe unayotumia katika taasisi yako ya elimu; iwapo huna barua pepe ya taasisi au mfumo hauikubali, tumia chaguo maalumu kwa waombaji wasio na barua pepe hiyo.

(ii) Tengeneza Kitambulisho cha Omnicampus kwa kutumia anuani yako binafsi ya Gmail na wasilisha Kitambulisho cha Mwanafunzi au nyaraka nyingine rasmi zinazothibitisha udahili wako.

(iii) Baada ya usajili kukaguliwa na kuidhinishwa, utapokea taarifa za kuingia kwenye mfumo wa Omnicampus.

(iv) Ingia kwenye mfumo, chagua “GCI World 2026 September” na ukamilishe maombi.

**Taarifa zaidi na maombi:** https://weblab.t.u-tokyo.ac.jp/en/lecture/gci/

**Ubalozi unawahamasisha wanafunzi wenye sifa nchini Tanzania kutumia fursa hii muhimu ya kuongeza ujuzi katika teknolojia za kisasa za Sayansi ya Data na Akili Mnemba.**

**UBALOZI WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA NCHINI JAPAN**
**12 AGOSTI, 2026**